




SANAA YA UTONGOZAJI

*Namna ya Kuwa Mwanaume mwenye Mvuto
na Ushawishi kwa Mwanamke*

ISAACK NSUMBA

SANAA YA UTONGOZAJI

*Namna Ya Kuwa
Mwanaume Mwenye Mvuto
Na Ushawishi Kwa
Mwanamke*

-ISAACK NSUMBA-

HAKIMILIKI

Kitabu hiki kimeandikwa na Isaack Nsumba,
Kikiwa ni kitabu cha 12. Haki zote
zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili au
kudurufu sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya
mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji
wa haki za mwandishi na mchapaji.
Ikigundulika hatua kali za kisheria
zitachukuliwa.

Copyright 2022

Mawasiliano:

Isaack Nsumba

Dar es Salaam-Tanzania

www.isaacknsumba.com

YALIYOMO

YALIYOMO	3
SHUKRANI	4
UTANGULIZI	6
SURA YA KWANZA	11
MAANA YA KUTONGOZA NA AINA ZA UTONGOZAJI.....	11
SURA YA PILI	18
IJUE SAIKOLOJIA YA MWANAMKE WAKATI ANATAKA MWANAUME WA KUWA NAE	18
SURA YA TATU	29
IJUE KANUNI YA UTONGOZAJI INAYOFANYA KAZI ZAIDI.....	29
SURA YA NNE.....	47
MAKOSA YA KUEPUKA WAKATI UNAMTONGOZA MWANAMKE	48
HITIMISHO	56
KUHUSU MWANDISHI	63

SHUKRANI

Mafanikio katika maisha ya kila mtu huwa yanachangiwa na watu wengi sana. Ningependa kuishukuru familia yangu, Mpenzi wangu Rebecca kwa sapoti yake isiyoisha kuhakikisha ananitia moyo na kunipa muda wa utulivu kufanya kazi za uandishi kwa ajili ya kusaidia watu wengi.

Ili kuhakikisha kuwa kitabu hiki kinakuwa bora zaidi, Baraka Kasinge, mhadhiri msaidizi, CHUO KIKUU cha SAUT-MTWARA ambae amefanya kazi kubwa kama muhariri mkuu wa kukipitia na kuweka nyongeza muhimu ili kumsaidia msomaji afaidike zaidi, ubora unaouona humu ni matokeo ya mchango wake.

Timu nzima ya Nsumba Creative Media ikiongozwa na Gasper kilenga. wanastahili pongezi kwa kushughulikia usanifu wa jarada

la kitabu hiki ili kiweze kukufikia mkononi mwako kikiwa na sura nzuri.

Familia nzima ya Love Academy ambayo mmeniamini hata kunifanya kuwa mwalimu na mwanafunzi pamoja nanyi, uwepo wenu umenifanya niwajibike kuhakikisha najinoa ili niendeleo kuwasaidia kiufahamu na maarifa.

Watu wote ambao mmenipa nafasi ya kuwafundisha kwa njia ya moja kwa moja au kupitia mtandao, Kila nilipoitumia nafasi mliyonipa mlinisaidia kunoa ujuzi na maarifa yaliyopelekea kitabu hiki kuandikwa.

UTANGULIZI

Mwanasaikolojia nguli Bwana Lev Vygotsky alifanya utafiti ili kubaini aina 70 za hofu zinazowakumba wanadamu, katika utafiti wake alikuja kubaini kuwa asilimia 80 ya wanaume wana hofu ya kuzungumza na wanawake ambayo kitaalamu inafahamika kama “Gynophobia”, hii ni kusema kwamba wanaume 8 kati ya wanaume 10 hawana ujasiri kabisa wa kuzungumza na wanawake na wana hofu ya kufanya hivyo.

Alipokuwa akiendelea kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha wanaume kuwa na hofu hiyo alikuja kupata majibu ya kushangaza sana ambayo hata wewe leo yanaweza kukushangaza pia.

Katika utafiti wake alibaini kuwa wanaume wengi wana hofu ya kuzungumza na wanawake sio kwa sababu hawana uwezo wa kufanya hivyo ila ni kwa sababu hawajui saikolojia ya mwanamke na Sanaa ya utongozaji itakayomsaidia mwanaume kuwa na ujasiri wa kuzungumza nao, kisaikolojia imethibitika kuwa wanawake ni viumbe wanaopenda kusikilizwa na kusikiliza hata kama wao wanaongea au wanaongelehwa vitu visivyo na maana yoyote, pamoja na wanaume wengi kuujua huu ukweli kuwa haihitaji mambo mazito ili waweze kuongea na mwanamke bado idadi ya wanaume wenye uwezo wa kufanya hivyo imekuwa ndogo sana.

Tafiti zilizofanywa hivi karibuni zimebaini kuwa kadri siku zinavyozidi kwenda ndivyo hofu hii huzidi kuwakumba wanaume wengi na ndio maana wengi hupendelea kuomba namba ya simu na sio kuwasilisha uhitaji wao kupitia

mdomo, matokeo ya utafiti yamebaini kuwa hata baada ya wanaume kupewa namba bado hofu ya kuwasiliana na mwanamke huwa palepale kwa kutokujua namna sahihi ya kuelezea hisia zao na kuonesha uhitaji.

Yawezekana hata wewe umewahi kutamani kukutana na mwanamke mzungumze ila alipokubali wito wako na mlipokutana maneno ambayo ulipanga kumwambia yalitoweka na ujasiri ukapotea kabisa mbele yake, au uliomba namba ya simu na mara baada ya kupewa ulijikuta hauna cha kumwambia ili kumfanya ajue, ashawishike na kukukubalia uhitaji wako.

Kuwasilisha uhitaji wako kwa mwanamke ni jambo linalohitaji ufahamu mkubwa kwa sababu lengo lako ni kugusa hisia zake na

kumfanya akuone wewe unamfaa, ufahamu huo nimeuita “SANAA YA UTONGOZAJI”

Lengo la kitabu hiki sio kukufanya uwe mwanaume wa kila mwanamke, ila kimedhamiria kukujaza ufahamu utakaokusaidia kutimiza lengo la kuwasilisha hisia zako kwa mwanamke unaemtaka kwa sababu kama ukishindwa kufanya hivyo ni rahisi sana kuingia katika mahusiano na mwanamke usiyemtaka kwa sababu tu ulishindwa kumpata yule umtakea kwa kutokujua namna ya kuelezea hisia zako kwake.

Karibu ujifunze.

Isaack Nsumba

SURA YA KWANZA

MAANA YA KUTONGOZA NA AINA ZA UTONGOZAJI

Kutongoza kunaweza kukawa na maana na tafsiri nyingi, mwisho maana na tafsiri hizo lazima zikutane mahali pamoja na kukubaliana kuwa; *Kutongoza ni kitendo cha kuwasilisha hisia za uhitaji wa kuanzisha mahusiano na mtu wa jinsia ya tofauti na yako ili kumfanya ashawishike kuwa nawewe.*

Lengo la uwasilishaji wa hisia hizo za uhitaji ni kumshawishi unaemtaka na kumfanya aone kuwa wewe unafaa kuwa nae na kutokea hapo awe tayari kuwa nawewe. Kutongoza ni zaidi ya kumwambia mwanamke kuwa “Nakupenda, nataka nikuo tujenge familia”

Kutongoza ni Sanaa na Sanaa ni ufundi wa kufanya jambo fulani katika namna ya uzuri na mvuto kiasi cha kumvutia mtu mwingine, wapo wanaume wamekosa wanawake sio kwa sababu wanawake hao hawakuwa sahihi ila kwa sababu walikosa au kupungukiwa uwezo wa kushawishi, ili mwanamke akubali kuingia katika mahusiano nawewe anahitaji kupata sababu ya kwanini afanye hivyo na sababu hiyo anatakiwa aipate kutoka katika ushawishin wako.

Kama usipokuwa na uwezo wa kumshawishi mwanamke kuna hatari ya kukosa mwanamke unaemtaka na kuangukia katika mikono ya mwanamke ambae humtaki ila kwa sababu amekuja mwenyewe au umetafutiwa, kuna msemu unasema kuwa “kuna kula unachokitaka na kula unachokipata”

Mtu anaejua namna ya kukipata kile anachokitaka yupo katika nafasi nzuri ya kukipata, mtu asiyejua namna ya kukipata anachokitaka ni vigumu sana kukipata hata kama alistahiri kukipata.

Kuna mwanamke fulani ni haki yako kabisa kuwa nae ila kwa sababu umekosa uwezo wa kumshawishi basi ni vigumu sana kumpata, hii ni kwa sababu hata kama anakupenda bado atahitaji ushawishi wako, kwa kufanya hivyo ndivyo hujisikia raha na kuona umemtendea haki.

Kutongoza kumegawanyika katika aina mbili, ya kwanza ni **VERBAL SEDUCTION** ambapo inakutaka mwanaume kumueleza mwanamke kwa maneno juu ya hisia na uhitaji ulionao wa kuingia katika mahusiano nae, aina hii ya

utongozaji ndio iliyozoeleka na kutumiwa na wengi.

Katika aina hii ya utongozaji, kilicho na umuhimu ni ujasiri wa kuongea na uwezo wa kuyapangilia maneno ili kuwasilisha ujumbe wako kwa mwanamke unaemtaka na wenye uwezo mzuri wa kufanya hivyo huwa wanafanikiwa, aina hii ya utongozaji huweza kufanyika ana kwa ana au kupitia simu kwa njia ya meseji au maongezi.

*“Basi Dina, binti Lea, ambaye Lea alimzalia Yakobo, akatoka kuwaona binti za nchi. 2 Shekemu, mwana wa Hamori, Mhivi, mkuu wa nchi, akamwona akamtwaa, akalala naye, akambikiri. 3 Moyo wake ukaambatana na Dina binti Yakobo, **akampenda huyu msichana, akasema na huyu msichana kwa***

maneno mazuri.” Mwanzo 34:1-2

Aina ya pili ya utongozaji inaitwa ***NON-VERBAL SEDUCTION***, katika aina hii ya utongozaji mwanaume hulazimika kuwasilisha uhitaji wake kupitia vitendo vya wazi (communicating through acts of services) aina hii ya utongozaji imeambatana na gharama ya muda, fedha pamoja na utayari, hii ndio aina ambayo nashauri watu wengi waitumie kwa sababu imethibitishwa na wanasaikolojia kuwa hakuna kitu kinapeleka ujumbe kwa haraka katika ubongo wa mwanadamu kama matendo anayotendewa, hautakiwi kumwambia mtu vile unamjali na kumthamini anaweza kuyaona hayo kupitia matendo yako, kupitia matendo yako ndipo mwanamke huweza kujua namna unavyomjali na kumthamini na ndio maana ni rahisi sana mwanaume kumteka mwanamke ambae ameolewa ikiwa atafanikiwa kumfanyia yale ambayo hafanyiwi na mume wake.

Kilicho na umuhimu katika hii aina ya pili ni kujua matendo ambayo ukimfanyia mwanamke unaemtaka yataachilia mguso “affection” ndani yake na kumfanya akuhitaji au aone kuwa wewe unamfaa kwa sababu unajua kugusa hisia zake.

Kumbuka, kutongoza ni zoezi linalolenga kushawishi, ili uweze kumshawishi ni lazima uguse katika vitu anavyovipenda bila yeye kukwambia, hii itakuongezea nafasi “credit” ndani ya moyo wake na kumfanya ajue kuwa unazijua hisia zake vizuri na unajali mahitaji yake, kwahiyo lengo sio tu kufanya, bali ni kufanya kilicho muhimu, katika ubora na kwa wakati kinapohitajika.

SURA YA PILI

IJUE SAIKOLOJIA YA MWANAMKE WAKATI ANATAKA MWANAUME WA KUWA NAE

Miaka ya 70 jopo la wanasayansi kutoka nchini China na Japan wakiongozwa na Masao Doi, Takuzo Aida, Yuen Ren Chao pamoja na Pan Jianwei walifanya utafiti kwa samaki wa kike anaeitwa “GOLDFISH” ili kubaini ni kitu gani ambacho samaki huyo anaangalia anapotafuta Goldfish wa kiume ili waweze kujaamiana.

Katika utafiti wao waliweza kubaini kuwa Goldfish wa kike anapotafuta Goldfish wa kiume huangalia Goldfish mwenye wanawake wengi au aliyezungukwa na wanawake wengi zaidi kuliko wengine.

Baada ya kugundua hilo ndipo walipokuja na matokeo ya utafiti wao ambao waliwasilisha kwa jina la “TRIANGLE OF HUMAN DEMANDS” ambapo walielezea aina tatu ya vitu ambavyo binadamu anavihitaji zaidi.

Kitu cha kwanza ni kile ambacho hawezi kukipata au ambacho hakipatikani kirahisi.

Binadamu wengi wanapenda vitu visivyopatikana kirahisi, hii ni kwa sababu binadamu asipopata changamoto katika kupata kitu kiwango chake cha furaha baada ya kukipata kitu hicho huwa kidogo sana na kuna uwezekano asikipe thamani inayostahili.

Kwa wanawake hii ipo, wanawake wengi hawapendi wanaume ambao wanapatikana

kirahisi na ndio maana mara nyingi mwanamke akijua unampenda anaanza kukudharau, kama utakuwa mfuatiliaji utakuja kugundua kuwa mtaani kwenu, shuleni au chuoni wanaume wanaoonekanaga kuwa bize na mambo yao huwa na nafasi kubwa ya kupata wanawake tofauti na wale ambao huwa karibu zaidi na wanawake, hii ni kwa sababu wanawake hawapendi au kuvutiwa na wanaume ambao wanapatikana kirahisi.

Kitu cha pili ni kile ambacho wengine wanakihitaji au kinahitajika zaidi “Most wanted”

Wanawake hawapendi wanaume ambao hawahitajiki, hii ndio sababu kwanini wanaume maarufu wanapendwa sana na wanawake pamoja na ukweli kwamba wanawake hao wanajua kuwa hawawezi kuwa peke yao hata wikipewa nafasi.

Mwanamke anajisikia fahari zaidi akijua kuwa yupo katika mahusiano na mwanaume ambae anahitajika na wanawake wengine na ndio maana mwanaume mwenye wanawake wengi ni rahisi zaidi kupata wanawake wengine kuliko yule asiye na mwanamke kabisa.

Ili kuthibitisha hili fuatilia wanawake wengi utakuja kugundua kuwa wapo tayari wakubali kuwa na mwanaume ambae ameo ila sio mwanaume ambae hana mwanamke, kwahiyo weka akilini mwako kuwa unatakiwa kumuonesha mwanamke kwamba kama atakupata wewe basi amebahatika sana kwa sababu idadi ya wanawake wengine wanaokuhitaji wewe ni kubwa sana.

Kitu cha tatu ni kile ambacho wachache tu ndio wana “access” nacho.

Moja ya jambo muhimu unalotakiwa kulijua kuhusu wanawake ni kwamba Wanawake wanahitaji wanaume ambao sio kila mwanamke anaweza kuwapata japo wanahitajika zaidi (*Most of women feel attracted to men who are highly demanded but can't be cheaply available*)

Hii ndio sababu kwanini mwanamke anaweza kuvutiwa kirahisi na mwanaume ambae anajua kuwa atakuwa pekeake, lakini pia wanawake wenzake watakuwa wanamuonea wivu kwa sababu ya nguvu ya ushindani, Nguvu na uhitaji na wivu (Power of competition, Demand and Jealousy)

Mwisho kabisa utafiti wa wanasayansi hao ulihitimisha kwa kusema kuwa Mwanamke

anahitaji mwanaume ambaye Hawezi kumpata, anayehitajika na wanawake wengi zaidi pamoja na mwanaume ambaye hapatikani kirahisi.

Hii ni kusema kwamba mwanamke akikupa namba ya simu saivi na ukamtafuta muda huohuo umekosa kigezo cha kuwa nae.

Hii ina maana kwamba ukimuonesha mwanamke kuwa hakuna mwanamke mwingine anaekutaka basi tayari umekosa nguvu ya kumpata, hii ni kusema kwamba mwanamke akijua kuwa hakuna mwingine anaekuhitaji basi umeshamkosa.

Unajua ni kwanini? Hii ni kwa sababu zifuatazo.

1. Wanawake wengi huamini kuwa mwanaume mzuri ni yule ambae wanawake wengi wanamtaka, yawezekana asiwe mzuri mbele ya macho ya mwanamke huyo, ila kwa sababu tu wanawake wanaomtaka ni wengi basi kuanzia hapo ataanza kumuona mzuri.
2. Watu wengi huamini kuwa kitu kinachohitajika zaidi ni kizuri na kina thamani kubwa, hii ipo hata kwa wanawake wakati wanaangalia mwanaume wa kuwa nae, wengi huangalia idadi ya wanawake wanaomuhitaji mwanaume huyo na ndio maana mwanamke yupo tayari kumuacha mwanaume ambae kwake yupo pekeake na kwenda kwa mwanaume ambae atakuwa na mwanamke mwenzake.

3. Wanawake wengi wanaendeshwa na udadisi (Driven with curiosity) mwanaume akiwa anasifiwa au anaonekana kuwavutia wanawake wengine wanawake huanza kujiuliza ana kitu gani cha tofauti na wanaume wengine? Swali hili linaibua uhitaji wa kutaka kuwa karibu na mwanaume huyo na kuanzia hapo huanza kujenga matamanio ya kuwa nae.
4. Moja ya kitu ambacho wanawake wengi wanakitafuta ndani ya mwanaume ni uhakika “Assuarance” na uhakika huu hakuna namna wanaweza kuupata isipokuwa kwa kuwaangalia wanawake wanaomzunguka mwanaume huyo.

Hii tafsiri yake ni kwamba mwanamke anapomtazama mwanaume mwenye mwanamke anapata kufahamu kuwa mwanaume huyu ana uwezo wa

kumridhisha mwanamke na kumtunza na ndio maana akapendwa, anapata kujua kuwa mwanaume huyu ni mwanaume anaefaa na ndio maana kuna mwanamke alimkubalia, kwahiyo mwanaume unapomtongoza mwanamke epuka sana kumuonesha kuwa upo single, hiyo itamfanya ajiulize maswali mengi kama huyu mwanaume ana kasoro gani mpaka anakuwa single?

Kwahiyo, unatakiwa kufahamu kuwa kuna thamani fulani ambayo mwanamke anaitafuta ndani ya mwanaume na sio tu lile umbile lako la kiume.

SURA YA TATU

IJUE KANUNI YA UTONGOZAJI INAYOFANYA KAZI ZAIDI

Dan Bilzeriani ni miongoni mwa wanaume maarufu sana duniani, na umaarufu huo amejipatia kutokana na uwezo wake mkubwa wa kunasa wanawake wazuri Zaidi duniani, kwa sasa anajulikana kama “Playboy” wa Dunia.

Lengo la sura hii sio kukufanya uwe playboy ila kuna kitu kizuri cha kujifunza kutoka kwa Dan ambacho kimeandikwa pia katika kitabu cha

Dominick Mann kinachoitwa UNLOCK HER LEGS (Namna ya kumvutia mwanamke bila kutumia nguvu wala gharama kubwa) na kitu hicho ni kanuni ambayo mimi nimeipa jina la **“DON’T CHASE, JUST ATTRACT”** (Usifukuzie, Vutia)

Kanuni hii inasema kwamba, kadri unavyojitahidi kumfuatilia mwanamke na kumuonesha kuwa unamuhitaji sana ndivyo unavyoidi kumfanya apoteze hamasa ya kuwa nawewe na aanze kukupuuzia (*loose interests and start ignoring you*)

We mwenyewe ni shahidi katika hili, mwamnamke ambae umekuwa ukijitahidi kadri uwezavyo kumuonesha jinsi unavyomuhitaji na kumthamini ndiye anaekuumiza na kukupuuzia kana kwamba haoni juhudi na jitihada zako kwake.

Hii ni kwa sababu wanawake hawataki wanaume “cheap” wanahitaji wanaume ambao wanahitajika zaidi na hawapatikani kirahisi kama tulivyoangalia katika sura ya pili.

Kwahiyo kwa mujibu wa kanuni hii kuna mambo kadhaa ambayo mwanaume anatakiwa aepuke wakati anamtongoza mwanamke.

Jambo la kwanza, epuka kumuonesha kuwa unamuhitaji zaidi.

Hii kanuni inasema kwamba kadri unavyomuonesha kuwa unamuhitaji ndivyo ambavyo thamani yako kwake inashuka na ukumbuke thamani yako ikishuka unapoteza mvuto na ukipoteza mvuto unakosa ushawishi

ndio maana unaweza kujitahidi kumuonesha kuwa unampenda na wala asijali kabisa juhudi zako.

Siri ya kuwa na nguvu na mvuto kwa mwanamke ni kumuonesha kuwa haumuhitaji kama ambavyo anadhani na unaweza kufanikiwa katika hili kwa kumuonesha au kumuaminisha kuwa una machaguo mengi zaidi (more options) na sio yeye pekeake, hii itamfanya ajue kuwa kama asipokupa nafasi na kukuwahi wewe basi wengine watamuwahi kwa kukupa nafasi. *(The secret of having power over women is not to show that you need them)*

Akifika hiyo hatua ndani yake inazaliwa hofu ya kupoteza au kukosa nafasi ambayo inafahamika kama FOMO na hii itamfanya

akupe nafasi haraka iwezekanavyo ili asiye akakukosa wakakuchukua wengine.

Jambo la pili, Epuka kumuonesha kuwa una chaguo moja tu ambalo ni yeye pekeake.

Katika sura ya pili tuliangalia namna ambavyo samaki jike aina ya Goldfish anavyovutiwa na samaki dume mwenye wanawake wengi ndivyo ilivyo kwa mwanamke, mwanamke akijua kuwa hauna options zaidi yake ni vigumu sana kumpata, na miongoni mwa kauli ambazo hutakiwi kabisa kumwambia ni kauli kama “sina mwingine zaidi yako, ukinikataa wewe nani atanitaka” na zingine zinazofanana na hizo.

Moja ya mbinu ya kufanikiwa katika hilo ni kutokukubali kuwa hauna mwanamke mwingine, muoneshe kuwa kama yeye

akikataa unao uwezo wa kumpata mwingine aliye bora zaidi, hii itamfanya ajue kuwa wewe ni wa thamani na unahitajika jambo ambalo linaweza kumshawishi na yeye kukuhitaji.

Jambo la tatu, Epuka kumuonesha kuwa wewe unapatikana kirahisi.

Wakati unamtongoza mwanamke epuka kumfanya akuone wewe ni “Cheap” na badala yake jibidiishe kumfanya ajue akipata nafasi ya kuwasiliana nawewe au akipata muda wa kuzungumza nawewe iwe ni kupitia simu au ana kwa ana basi anatakiwa kujua kuwa amepata nafasi ya upendeleo sana, inashauriwa kukaa masaa 12 kuanzia ulipopata namba ya mwanamke uliyekutana nae kabla ya kuwasiliana nae kwa mara ya kwanza.

Wengi huwa wanafanya kosa la kutuma meseji au kupiga dakika chache mara baada ya kupewa namba, hii inamfanya akutafsiri kuwa wewe ni cheap na ni mrahisi mbele yake, kinachotokea anapata nguvu juu yako jambo ambalo sio sahihi.

Kumbuka kuwa kiasili binadamu anapenda kukutana na ugumu utakaomuumiza kichwa na ndio maana kuna wakati uwezekano wa kupata kitu fulani kirahisi upo lakini mtu anatumia njia yenye ugumu kidogo, mwanamke anataka mwanaume ambae atamsumbuasumbua na kumfikirisha na sio mwanaume ambae ni mrahisi, akikupa namba hakikisha unajifanya kama umesahau ili ajue kuwa haumzingatii na kumtilia maanani, hii itamfanya awe na jukumu la kuitafuta “attention” yako na akiipata anajiona mwenye bahati.

Jambo la nne, Epuka kumuonesha kuwa kutokuwepo kwake kuna athari katika maisha yako.

Kwa mujibu wa hii kanuni inasema kuwa kadri unavyomuonesha mwanamke kuwa una furaha hata bila ya uwepo wake ndivyo unavyozidi kumfanya akufuatilie na aweke umakini wake kwako (put her attention into you) ili apate nafasi ya kujua ni kitu gani kinachokupa furaha.

Ile attention atakayoweka kwako inalenga kutaka kujua ni kwa namna gani unampenda na wakati yeye sio chanzo cha furaha yako kwa sababu hata asipokuwepo wewe una furaha, swali hili linaweza kumpa majibu kuwa yeye kwako sio kipaumbele kwa sababu una machaguo mengine ndio maana una furaha, hii inaweza kumfanya awe dhaifu na mwenye

kunyong'onyea kwa sababu anajua kuwa kwako hana nafasi kubwa, akifika hii hatua ni rahisi sasa wewe kumpata kwa sababu ataona kama amependelewa kuwa nawewe.

Wanaume wengi wanakosea sana kuwaambia wanawake maneno kama “sijalala, sijakula au sijafanya kitu fulani” wakiadini kuwa maneno hayo huashiria upendo wasijue kuwa maneno hayo hutosha kumfanya mwanamke awaone wao ni wadhaifu.

Kumbuka kuwa wanawake wanavutiwa na wanaume walio imara, wanaojiamini na wanaume ambao hawawezi kuendeshwa wala kuathiriwa kihisia, hii humfanya mwanamke ajione yuko sehemu salama ikiwa atapata nafasi ya kuwa na mwanaume huyo.

NAMNA YA KUITUMIA KANUNI YA “DON’T CHASE, JUST ATTRACT” KUMPATA MWANAMKE UNAEMTAKA

Kwa sababu kanuni inasema unatakiwa uwekeze nguvu nyingi kumvutia mwamnamke unaemtaka na sio kuwekeza nguvu nyingi kumfukuzia basi kuna mambo unatakiwa kuyafanya ambayo yatakusaidia kumfanya avutiwe nawewe na akivutiwa nawewe ni rahisi wewe kumshawishi na kumfanya awe mwenzi wako.

Jambo la kwanza; Muoneshe kuwa unahitajika na wengi.

Mfano wa samaki jike unatuonesha kwamba wanawake wanahitaji wanaume ambao

wanahitajika na wanawake wengi, njia mojawapo ya kumvutia mwanamke ni kumfanya ajue kuwa wewe ni aina ya mwanaume ambae unahitajika na wanawake wengi.

Dan Bilzerian anaetajwa kama mwanaume mwenye mvuto na ushawishi mkubwa kwa wanawake alipoulizwa aliwezaje kuwa na uwezo huo alibainisha kuwa kuna wakati ilimlazimu kufanya sherehe fupi na katika sherehe yake huwaalika wanawake ambao atapiga nao picha na kisha kupost katika kurasa zake za mitandao ya kijamii.

Hii iliwafanya wanawake kujawa na wivu kwa kudhani wanawake walio karibu na Dan kuna kitu wanafaidi, lakini pia hali hii ilibua udadisi “Curiosity” ndani ya wanawake na kujiuliza Dan alikuwa na kitu gani cha kipekee kiasi cha kuvutia wanawake wengi namna hiyo?

Hii ilimtengenezea mazingira ya kuwavutia wengine na kuwafanya watamani kuwa karibu nae jambo ambalo liliwafanya waanze kutafuta umakini “attention” wake na baada ya muda ni wanawake ndio walikuwa wakimfukuzia Dan na sio Dan kuwafukuzia wao.

Sisemi ufanye kama Dan, ila nataka uone namna ambavyo ukifanikiwa kumfanya mwanamke ajue kuwa wewe ni mwanaume unaeyehitajika sana “The most wanted man” utafanikiwa kumfanya yeye avutiwe nawewe.

Jambo la pili; *Tumia pre-selection rule.*

Pre-selection ni shiria inayosema kuwa ili uweze kumpata mwanamke unaemtaka ni vizuri kutafuta mwanamke ambae kupitia huyo unaweza kufanikisha zoezi lako la kumvutia umtakae.

Hii ni kusema kwamba, yawezekana una rafiki wa kike ambae mmezoana nae, unaweza kumtumia huyo kama sehemu ya kujitangazia ili kumvuta unaemtaka, unaweza kulifanikisha hilo kwa kutumia muda mwingi pamoja nae huku mkifurahia, unaweza kumjali ili kumfanya yule umtakae apate wivu na aanze kukuhitaji wewe.

Mtu mmoja aliwahi kusema kuwa mwanaume aliye na mpenzi na akampenda mpenzi wake kwa wazi anao uwezo wa kupata wapenzi wengine wengi kwa sababu watavutiwa na vile mwanaume huyo anavyompenda mpenzi wake na kuwafanya wapatwe wivu, kwahiyo unaweza kumtumia rafiki yako wa kike kama jukwaa la kujinadi kwa mwanamke unaemtaka.

Kwa upande mwengine pre-selection inakutaka uweke ukaribu na rafiki wa mwanamke

umtaka na umfanye rafiki huyo kufurahia zaidi uwepo wako, unajua nini kitatokea ukifanya hivyo?

Kama ukiweka ukaribu na rafiki wa mwanamke unaemtaka na ukafanikiwa kumfanya afurahie basi utakuwa kwenye nafasi nzuri ya kumpata mwanamke umtaka kwa sababu atavutiwa na kile unafanya kwa rafiki yake na kujawa wivu ndani yake.

Utafiti umebaini kuwa hakuna wanaume wanaopata wanawake kirahisi kama wale ambao wana marafiki wa kike ambao wanafurahia urafiki huo au wenye wapenzi wanaofurahi na kupendeza, hii ni kwa sababu wanawake wanapenda wanaume wenye uwezo mkubwa wa kuwapa furaha, ikionekana mwanaume anaweza kumpa furaha mwanamke wake ni rahisi sana mwanaume huyo kuvutia wanawake wengine.

Jambo la tatu; tafuta thamani na uiuze *thamani yako. (Be the prize)*

Umeshawahi kujiuliza ni kwa nini kuna wanaume wanakimbiliwa zaidi na wanawake kuliko wanaume wengine?

Hii ni kwa sababu wanaume hao wana thamani fulani inayowafanya wanawake wavutiwe na hadhi “Status” fulani za wanaume hao, hii mana yake ni kwamba mwanamke anavutiwa zaidi na hadhi aliyonayo mwanaume.

Hadhi inatokana na mwanaume kufanya mambo fulani yanayokubalika katika jamii na ndio maana waigizaji, wacheza mpira, wachekeshaji, waimbaji na watu wanaofanana na hao huwavutia wanawake kirahisi zaidi kuliko wengine.

Kama una kipaji au uwezo wowote unaokufanya ufanye jambo fulani katika ubora wa hali ya juu utumie uwezo huo unaweza kukuongezea thamani kiasi cha kumfanya mwanamke akuhitaji.

Unachotakiwa kukumbuka ni kwamba lengo la kutongoza ni kujiuza na kuhakikisha unauzika kwa mwanamke unaemtaka na ili uweze kufanikiwa katika hilo lazima uwe vile ambavyo yeye atavutiwa nawewe.

SURA YA NNE

MAKOSA YA KUEPUKA WAKATI UNAMTONGOZA MWANAMKE

Wakati mwingine ugumu unaokutana nao katika kumtongoza mwanamke sio kwa

sababu hakutaki, ila ni kwa sababu kuna makosa ambayo unafanya yanayosababisha ashindwe kuvutiwa na wewe, hakikisha makosa haya unayaepuka kwa gharama yoyote ile.

Kosa la kwanza ni ***hali ya kumfanya awe rafiki***, mwanamke akikufanya wewe kama rafiki yake ni vigumu sana kugeuka na kuwa mpenzi, hii ni kwa sababu akiwa mpenzi wako ni vigumu sana kuwa rafiki.

Urafiki kati ya mwanamke na mwanaume humfanya mwanamke kujihisi huru kuelezea hisia zake na ndio maana anaweza akawa anakuelezea jinsi ambavyo anakutana na migogoro katika mahusiano na mwanaume wake.

Lakini pia fahamu kuwa wanawake kwa asili hutafuta kitu kilicho mbali na ambacho hawana

na ndio maana ni rahisi kwa mwanamke kuingia katika mahusiano na mwanaume asiyemjua na kukuacha wewe ambaye umekuwa rafiki au karibu yake kwa muda fulani.

Kosa la pili ni **kuwekeza kwajili yake au kujitoa zaidi kwake**. Nadhani umewahi kusikia wanaume walioachwa na wanawake waliowasomesha mpaka wakafika hatua ya kuhitimu, kinachomfanya mwanamke amuache mwanaume pamoja na gharama nyingi ambazo mwanaume ameingia ni kwa sababu kadri mwanaume anavyowekeza zaidi kwa mwanamke ndivyo ambavyo anazidi kupoteza mvuto mbele ya macho ya mwanamke huyo.

Kuwekeza ni aina mojawapo ya utongozaji kati ya zile mbili tulizoangalia katika sura ya kwanza, lakini unashauriwa usiwekeze katika kiwango cha kumfanya mwanamke ahisi

unataka kumnunua au kumteka kwa yale unayomfanyia.

Sababu ya pili ni kwamba wanawake wengi hawapendi kuwa watumwa au watu wanaotumikia kifungo fulani, unapowekeza zaidi kwa mwanamke inamfanya aone kama unataka kumtawala jambo ambalo litamnyima uhuru.

Sababu ya tatu, wanawake wengi wanamtafsiri mwanaume anaejitoa sana kwao kama mwanaume asiyejamini na ndio maana anatumia fedha na mali alizonazo kumteka mwanamke, kumbuka mwanamke yeyote anavutiwa zaidi na mwanaume anaejamini na ndio maana mwanamke anaweza kumuacha mwanaume mwenye fedha na kumfuata asiye na kitu kwa sababu tu mwanaume huyo anajiamini.

Kosa la tatu ni ***kumuonesha kuwa yeye ndiye chaguo lako la mwisho.***

Wanawake hawataki kabisa kujisikia wako katika mahusiano na mwanaume ambaye hana uwezo wa kupata mwanamke mwingine, hii inamfanya mwanamke afikirie kuwa upo nae kwa sababu hauna mwingine (Only option), wanawake wanapenda kujua kuwa miongoni mwa machaguo mengi uliyonayo umemuona yeye anafaa (The best option).

Hii inampa kujidai na kujiona ni mwanamke wa tofauti, wa thamani na mwenye bahati hata kukupata wewe, kwahiyo, usifanye kosa la kumuaminisha kuwa yeye ndiye chaguo lako la mwisho hata kama ukweli uko hivyo kwamba hauna chaguo jingine zaidi yake.

Kosa la nne ni ***kumuonesha kuwa kuna uwezekano wa wewe kuwa na mwanamke mwingine mara baada ya kuwa nayeye.***

Katika aina 70 za hofu zinazomkabili mwanadamu, kuna aina tatu za hofu zinamkabili zaidi mwanadamu mwenye jinsia ya kike.

Aina ya kwanza inaitwa **Anglophobia**, hii ni hofu ya kukutana na maumivu, mwanamke hayupo tayari kufanya jambo ambalo kabla hajalifanya atajua kuwa kuna uwezekano wa kukutana na maumivu, kwahiyo wakati unamtongoza epuka kumfanya ajue kuwa kuna uwezekano wa kumuumiza mbeleni kwa sababu akijua hivyo hawezi kukubali ili asikutane na maumivu.

Aina ya pili ya hofu inayowakumba wanawake zaidi inaitwa **chronophobia**, aina hii ya hofu humfanya mwanamke awe na hofu ya kukutana na mabaya, mabaya hayo yanaweza kuwa ni mateso na stress za mapenzi

utakazomsababishia, aina hii ya hofu wakati mwingine inafahamika kama “Assumed Danger” (hatari za kufikirika)

Hakikisha katika kila utakalofanya lengo lako liwe ni kumuhakikishia Amani, utulivu na usalama kwa muda wote atakaokuwa na wewe.

Aina ya tatu ya hofu inayowakumba wanawake inaitwa **Autophobia**, hii ni ile hali ya kuogopa kutelekezwa au kuachwa solemba, wakati unamtongoza mwanamke unatakiwa kumfanya ajue kuwa wewe na yeye mtakuwa pamoja katika nyakati zote, akijua kuwa kuna uwezekano wa kumtelekeza mbeleni labda baada ya wewe kufanikiwa ni vigumu sana kukupa wewe nafasi.

HITIMISHO

Kutongoza ni zoezi endelevu, hivyo sio zoezi la siku moja, mbili au wiki hii ni kwa sababu lengo lako ni kujenga Imani ndani ya mwanamke unaemtaka na kuuteka utayari wake.

Unachotakiwa kujua ni kwamba mambo madogo madogo unayomfanyia kila siku yana athari ambazo zitaonekana baada ya muda fulani, hii ni kwa sababu ya kanuni ya Brailfold inayoitwa “Aggregation of Marginal Gain” (kukusanya faida ndogndogo mara kwa mara.

Kanuni hii inasema ikiwa utawekeza juhudi zako kufanya jambo fulani kwa muendelezo

basi baada ya muda kuna uwezekano wa kufanikiwa katika jambo unalolifanya.

Yawezekana asikuelewe leo, lakini kama hautaacha wala kukata tamaa kuna siku atauona upendo wako na kutokea hapo ataanza kukuhitaji.

Baada ya kusoma kitabu hiki natamani kusikia shuhuda kutoka kwako vile kinaenda kukusaidia, usiache kutendea kazi kile ulichojifunza na uasiache kunipa mrejesho wa matokeo utakayoyapata.

Ahsante kwa kuwa umesoma mpaka mwisho.

Isaack Nsumba



LOVE ACADEMY

"A sensible guides to a fulfilling love relationship"

VITABU VINGINE

**Nimekuandikia vitabu vingine
vitakavyokusaidia kuongeza maarifa zaidi
pamoja na kukuimarisha wewe binafsi na
kuimarisha mahusiano yako**

1. SANAA YA KUTOA NA KUPOKEA
KATIKA MAHUSIANO

2. SANAA YA MAWASILIANO KATIKA MAHUSIANO
3. THE GOLDEN WOMAN
4. MANIFEST YOUR MANHOOD
(DHIHIRISHA UANAUME WAKO)
5. HISIA KIINI CHA MAFANIKIO
(EMOTIONAL MUSLES)
6. MWANAMKE MASHINE
7. BORESHA MAHUSIANO YAKO
8. MUACHE AENDE
9. MUONGOZO WA USOMAJI WA VITABU
10. HUYU NDIYE (MUONGOZO
UTAKAOKUSAIDIA KUMTAMBUA
MWENZI SAHIHI)

11. MAISHA NI KUSUDI (KWANINI
ULIZALIWA NA KWANINI BADO
UNAISHI?)

NB: Vitabu vyote vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na vipo katika mfumo wa pdf, unaweza kuvipata kupitia whatsapp au email, Ili kuvipata tumia mawasiliano **0654722733**.

**TEMBELEA MITANDAO YA KIJAMII YA
ISAACK NSUMBA**

YouTube: **Isaack Nsumba**

(Utapata VIDEO nyingi za kukufundisha mambo mbalimbali)

Instagram: **Isaack Nsumba**

(Utapata mafunzo kila siku yatakayokusaidia)

Facebook: **Isaack Nsumba**

(Utapata mafunzo kila siku na pia shuhuda mbalimbali.)

KUHUSU MWANDISHI

Isaack Nsumba, ni Mwalimu, Mwandishi na Mshauri wa masuala yote yanayohusu Mahusiano, Uchumba, Ndoa, pamoja na Malezi.

Ni Mbeba maono wa huduma inayoitwa “Wisdom For Winning Ministry” yenye lengo la kuwafanya watu wengi watembee na kuenenda kwa ufahamu, Maarifa, hekima na taarifa sahihi katika kutenda mambo. Ni mwanzilishi wa madarasa ya mahusiano kupitia mtandao “Love Academy Online Class”.

Ni mwanaume wa mwanamke mmoja anayeitwa Rebecca Isaack, amewahi kuwa kiongozi wa kanisa katoriki mkoani Iringa kwa muda wa miaka mitatu 2016-2018 akiwa kama

katekista, Ni mwalimu wa neno la Mungu akihudumu katika kanisa la International Evangelism Church Lenye makao makuu yake mkoani Arusha; kwa sasa anafanya kazi ya kutoa elimu ya mahusiano kupitia mitandao ya kijamii kama vile Whatsapp, Facebook, Youtube pamoja na Instagram.

Mawasiliano;

Email; nsumbaisaack@gmail.com

Text **+255 654 722 733**

Whatsapp **+255 654 722 733**